Powered by: www.manyamfranchise.com

SEHEMU YA A
Ufahamu

Suala ya nidhamu
Soma taarifa ifuatayo kisha jibu maswali yafuatayo.

Watu wengi hulinganisha adhabu na nidhamu. Wao huweka mipaka madhubuti ambayo ikikiukwa, matokeo ni adhabu kali. Adhabu aghalabu hutolewa kama malipo kwa kosa likishatendeka. Je, kuna njia nyingine? Dini hupendekeza kwamba kumuasa mwerevu ni heri kuliko kumchapa mjinga mara mia moja. Wataalamu wengi wanaashiria kuwa ikiwa ni lazima, basi kiboko kitumike tu iwapo njia nyingine zote zimeambulia patupu.

Wanaamini kwamba kuchapwa mara kwa mara hakubadili mienendo mibaya kuwa mema bali huendeleza dhana ya kwamba kosa ni kosa tu ikiwa litagunduliwa na adhabu kutolewa. Yaani mhusika hapati kuelewa umuhimu wa nidhamu bila ya kukadiria adhabu iambatanayo na uvunjaji wa sheria.

Kufunza nidhamu kwafaa zaidi kabla ya, kuliko baada ya, tendo kufanyika. Ni muhimu, kwa mfano katika shule zetu, wanafunzi kuelezwa yanayokubalika na yasiokubalika kataka mazingira yao. Kutiliwa mkazo umuhimu wa kutii na kutenda wema kuliko kutoa adhabu mtu anapokosa. Mambo mengi yaweza kufunzwa kwa kusisitika manufaa ya kuwa na nidhamu bora. Kwa mfano, mwanafunzi akitenda wema, asifiwe na kuhimizwa kushukilia mkondo huo. Hili litendwe hadharani. Kwa upande mwingine, ukosefu wa nidhamu usipewe nafasi ya kunawiri bali ukomeshwe haraka iwezekanavyo. Wanafunzi, kupitia kwa ushauri wa mara kwa mara, wahimizwe kujieleza kupitia kwa matendo maovu. Wapewe uhuru kwa kuzungumzia hofu, mahitaji na matarajio yao. Wahusishwe katika kuamua mambo yanayowahusu.

Kuna aina nyingi za adhabu iwapo itabidi tabia au matendo fulani kukomeshwa. Lililo muhimu ni kwamba mwanafunzi aelewa kuwa ametenda kosa na sharti aadhibiwe. Hasa ni muhimu adhabu ilingane na kosa. Mwanafunzi asiyekamilaisha kazi yake darasani, kwa mfano, aweza kunyimwa nafasi ya kushiriki michezoni kwa muda hadi kuwe na mabadiliko. Mwanafunzi mchokozi aweza kutengwa na wengine ili aone umuhimu wa utangamano.

"Adhabu ya kiboko karibu itapitwa na wakati wasema baadhi ya wataalamu," haitekelezi lolote. Je na wanafunzi sugu, wafanyweje? Upotovu wa nidhamu una mipaka yake. Ikibidi, mwanafunzi aweza kufukuzwa kwa muda au kabisa ili kuwaokoa wengine shuleni. Nazi mbaya harabu ya nzima.

Kwa upande wake, serikali inapendekeza sana ushauri. Ukosefu mwingi wa nidhamu hutokea kama njia ya mwanafunzi kutaka kudokezea hisia zake. Yafaa kufanywa uchunguzi kabla mwanafunzi kama huyu kuadhibiwa. Isitoshe, kiboko kikitumiwa kupindukiwa sugu, haambiliki hasemezeki. Kibiko kikiuka mipaka, hudhuru badala ya kusiaidia.

Maadamu nyakati zimebadilika, nidhmamu na adhabu zitatekelezwa kama mambo mawili mbalimbali au waonaji?

<u>Maswali</u>

a) Kuna tofauti gain kati ya adhabu na nidhamu? (alama 2)

.....

.....

.....

b) Taja njia mbali mbali za kurekebisha tabia kama zilivyojitokeza katika taarifa. (alama 3)

Powered by: www.manyamfranchise.com

.....

b) Tunga sentensi kudhihirisha maana yafuatayo. (alama 3)

i. Kiburi

.....

.....

ii. Kaburi

.....

.....

c) Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo. (alama 4)

Safiri _____ _____

Unda _____ _____

d) Kanusha sentensi hii.

Yeye angeniazima kalamu ningemaliza kazi kwa wakati. (alama 2)

.....

.....

e) Tumia visisitizi vya karibu kukamilisha sentensi zifuatazo. (alama 2)

i) Mwanafunzi..... ameadhibiwa jana na leo

ii) Mitume ..... ndio walioneza dini hapa.

f) Bainisha aina ya vitenzi katika sentensi zifuatazo. (alama 2)

i) Mimi ninakula chakula kitamu

.....

ii) Waithera ni msichana mkarimu

.....

g) Tofautisha kimaana jozi zifuatazo za maneno. (alama 4)

i) Suka Shuka

.....

.....

ii) Bamba Pamba

.....

.....

h) Bainisha viwakilishi katika sentensi zifuatazo na ueleze ni vya aina gani. (alama 4)

i. Kizuri kimenunuliwa dukani

.....

ii. Cha mlevi uliwa na mgema

.....

iii. Mwenyewe amejaribu kupigania haki zake

.....

iv. Wengi wamechelewa kuingia darasani

.....

i) Eleza matumizi ya neno 'Yule' katika sentensi zufuatazo. (alama 2)

i. Yule hapendi uvivu

Powered by: www.manyamfranchise.com

.....

.....

.....

c) Kuna ama mbali mbali za adhabu. Toa mifano miwili kutoka kwenye taarifa na miwili yako mwenyewe. (alama 4)

.....

.....

.....

.....

.....

d) Je, wanafunzi wachapwe viboko? Toa maoni yako. (alama 2)

.....

.....

.....

e) (i)Methali "Nazi mbovu ni harabu ya nzima " inahusianaje na ufahamu huu? (alama 1)

.....

.....

(ii) Kamilisha methali hizi. (alama 3)

1) Mchelea mwana kulia .....

.....

2) Mtoto umleavyo .....

.....

3) Adhabu ya kaburi .....

.....

f) Eleza maana ya: - (alama 5)

(i) Kumlasa

.....

(ii) Kunawiri

.....

(iii) Zimeambulia patupu

.....

(iv) Kukiuka mipaka

.....

(v) Haambiliki hazemezeki

.....

SEHEMU YA B

Matumizi ya Lugha

a) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo.

- Alimchinjia mgeni mbuzi (alama 2)

.....

Powered by: www.manyamfranchise.com

.....

ii. Mwanafunzi yule hapendi uvivu

.....

j) Tumia alama zifuatazo za kuakifisha katika sentensi kuonyesha matumizi yake. (alama 3)

i. Nukta za dukuduku

.....

ii. Ritifaa

.....

iii. Alama ya hizi

.....

k) Ainisha sentensi zifuatazo. (alama 4)

i. Mwanafuzi yeyote hodari atachaguliwa

.....

ii. Yohana alishinda tuzo nzuri

.....

l) Kamilisha tanakali za sauti zifuatazo. (alama 3)

i. Nyoka

.....

ii. Loa

.....

iii. Kamatana

.....

m) Onyesha kikundi nomino (KN) na kikundi tenzi (KT) katika sentensi zifuatazo. (alama 2)

i. Yeye alikamatwa akifanya maovu.

.....

ii. Kamau na Kadogo wamekwenda Kisumu kumtembelea nyanya yao.

.....

n) Andika sentensi zifuatazo katika usemi wa taarifa: (alama 2)

i. "Nyinyi mmekuwa hapa kwa muda gani?" Daktari aliuliza.

.....

ii. "Tafadhali Selele, usimwambie Ali niloyokwambia," Rashid alisema

.....

o) Maneno MKE WAKE yakifupishwa huwa ni MKEWE. Fupisha NYUMBANI MWAKE. (alama 1)

.....

.....

SEHEMU YA C

Fasihi Simulizi

a) Eleza maana ya hadithi zifuatazo. (alama 2)

i. Mighani

.....

Powered by: www.manyamfranchise.com

.....

.....

ii. Hekaya

.....

.....

.....

b) Eleza umuhimu wa fasihi simulizi katika jamii. (alama 5)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

c) Kamilisha vitendawili vifuatavyo. (alama 3)

i. Tunda langu la ajabu, juu nyama, katikati ngozi na ndani mahanga

.....

.....

ii. Nimelala lakini natazama sinema

.....

.....

iii. Mwanangu anakwenda mchena kutwa bila ya miguu, wala hachoki

.....

.....

Powered by: www.manyamfranchise.com

KISWAHILI MAJIBU YA KUSAHIHISHA FORM 2

SEHEMU YA A:
MAJIBU
a) Nidhamu – kule kuweza kuzingatia yakupasayo kufanya bila kuangaliwa wala kuogopa kuadhibiwa
Adhabu – malipo apatayo mtu kwa kuvunja sheria
b) – Kuwaza na kuwashauri wanafunzi juu ya manufaa ya kuwa na nidhamu
- Kuwahimiza wajieleze kwa maneno kuliko kwa matendo
- Kuadhibu kulingana na kosa lilotendwa
c) – Mkosoyi kunyimwa uhuru
- Mchokozi kutengwa na wengine
- Kunyimwa kushiriki michezoni
- Kufukuzwa kwa muda au kabisa
(Hakiki mifano miwili yake mwanafunzi) 2x1=2
d) (Hakiki mami ya wanafunzi)
e) Mwanafunzi mwenye matendo maovu aweza kuhaifu au kuathiri wengine vibaya
1.Hulia mwenyewe
2.Ndivyo akuavyo
3.Ajuaye maiti
f)(i) Kumwonya/kumkataza
(ii) Kuendelea vizuri, kupata mizizi
(iii) Hazikufanikiwa
(iv) Kufanya mambo kupitia kiasi
(v) Hasikii kabisa

SEHEMU YA B
a)– Alichinja kwa niaba ya mgeni
- Alichinja kwa sababu ya mgeni ili ale mbuzi
b)(a) Maringo
(b) Sio mbali kwa wakati au mahali
(c) Mahali panapo zikwa wafu
c) Usafiri Msafiri
Uundaji Muundo
d)Yeye asingeniazima kalamu nisingemaliza kazi kwa wakati
e)(i) Yuyu huyu
(ii) Wawa hawa
f) (i) Ninakula – Kitenzi halisi
(ii) Ni kitenzi kishirikishi kipungufu
g) (i) - Tengeneza nywele kwa mtindo Fulani
-Tikisatikisa kitu kiowevu
-Toka mahali juu ukielekea chini
-Kitambaa kikubwa kinachotandikwa kitandani
(ii)- Kamata ghafla na kwa nguvu
- Bati/kitu chembamba
-Sufi nyeupe inayotengeneza nguo
-Visha mavazi mazuri na ya kupendeza
h) (i) Kizuri – kiwakilishi cha sifa
(ii) Cha – kiwakilishi cha a – unganifu
(iii) Mwenyewe – kiwakilishi cha a – unganifu
(iv) Wengi – kiwakilishi cha idadi
i) (i) Kiwakilishi
(ii) Kivumishi
j) (i) ....
(ii) '
(iii) !
k) (i) N V V T
(ii) N T N V
l) (i) Twaa
(ii) Rovurovu/chepechepe
(iii) Papatu papatu
m) (i) KN KT
(ii) Kamau na kadogo – KN
Wamekwenda kisumu kutembelea nyanya yao - KT
n) (i) Daktari alitaka kujua walikuwa pale kwa muda gain
(ii) Rashid alimsihi Selele asimwambie Ali aliyomwambia
o) Nyumbaniwe

SEHEMU YA C:
FASIHI SIMULIZI
a) (i) Hadithi za kihistoria zinazoeleza kuhusu mashujaa wlioishi katika jamii Fulani
(ii) Aina ya hadithi ambayo mhusika mmoja huwafanyia wenzake ujanja
b) – Huelimisha
- Hufunza kuhusu maadili ya jamii
- Kuonya
- Kuhifadhi historia ya jamii
- Kuonyesha utamaduni wa jamii Fulani
- Kuwatazamisha wanajamii mazungira yao
c) (i) Firigisi
(ii) Ndoto
(iii) Jua